

Ujitokezaji wa Mbinu za Kibalagha katika Hotuba za Dkt. Samia Suluhu Hassan

Ahmad Y. Sovu¹

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.4>

Ikisiri

Balagha ni mbinu za matumizi ya lugha ambazo mzungumzaji huzitumia ili anachokiwasilisha kiwashawishi au kuwafurahisha wasikilizaji (TUKI, 2013). Kwa kawaida, uwasilishaji huo hufanywa kwa njia ya maandishi, mazungumzo, picha na kadhalika (Lupogo na Ambrosi, 2023). Shabaha ya makala haya ni kuonesha ujitokezaji wa mbinu za kibalagha katika hotuba za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan (kuanzia sasa Samia), ili kushawishi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Data za makala haya zimekusanywa maktabani kwa kupitia maandiko na pia uwandani kwa kuwahoji wanataaluma mbalimbali. Uchambuzi na uwasilishaji wa data za makala haya umeongozwa na Nadharia ya Balagha. Matokeo ya uchunguzi huu yanaonesha kuwa katika hotuba zake, Samia hutumia mbinu mbalimbali za kibalagha. Miongoni mwa mbinu hizo ni matumizi ya nafsi ya kwanza umoja na wingi, tafsida, misemo, vitambulisho hadhi, takriri, ufutuhi, masimulizi ya hadithi na kuchanganya msimbo. Pamoja na mambo mengine, mbinu za kibalagha hutumika kulainisha lugha katika kufikisha ujumbe wa uwajibikaji, kuonesha mshikamano na kutoa matumaini. Aidha, mbinu za kibalagha hutumika kulinda utu wa watu, kuisitiza juu ya masuala mbalimbali, kuhimiza maendeleo na kuonesha falsafa ya kiuongozi kwa wananchi. Makala yanatoa mchango wa kimbinu katika uga wa isimujamii hususani katika lugha na siasa, kwa kudhihirisha namna vipengele anuwai vya kibalagha na jinsi vinavyoweza kutumika katika hotuba za viongozi wa kisiasa na vikaleta taathira njema kwa jamii.

1.0 Utangulizi

Hotuba za kisiasa ni maelezo maalumu yanayotolewa na kiongozi mbele ya wananchi kwa ajili ya kufikisha ujumbe fulani. Hotuba za kisiasa, kwa kawaida, hutumia mbinu mbalimbali za lugha ili kufikisha ujumbe kwa walengwa kwa lengo la kuhamasisha na kushawishi umma. Dhamira ya hotuba za kisiasa ni kutoa athari za kihisia na kifikra kwa jamii ili kufikia malengo ya kisiasa kama vile kuungwa mkono au kuwahamasisha watu kuchukua hatua juu ya jambo fulani. Mbinu kuu inayotumiwa na wanasiasa katika hotuba zao ni matumizi ya balagha ambazo

¹ Barua pepe: sovu82@gmail.com

hujumuisha mbinu za kisanaa kama vile istiara (mipasho), majazi (mifano ya lugha) na tashihisi au tashititi.

Hotuba huundwa kwa sifa mbalimbali. Sifa hizo ni pamoja na lugha yake kuwa rasmi kwa sababu ya mchanganyiko wa watu wanaohutubiwa. Hotuba inakuwa na mfululizo wa mahadhi na mdundo wa kupendeza; huwa na matumizi ya maswali ya balagha, yaani maswali yasiyotaka majibu ya moja kwa moja. Hotuba hunuiwa kumfanya msikilizaji atafakari yanayosemwa kwa undani zaidi, haina kukatiza semi wala kusitasita isipokuwa mahali pa kupumua na kusisitiza; hutumia lugha shawishi mara nyingi na ni vizuri kutumia neno “sisi” badala ya “mimi” ili kuwahusisha waliopo katika maongezi yake. Hotuba hutumia methali au ucheshi kidogo ili kuwachangamsha wasikilizaji; huwa na marudiorudio ya sentensi au ya maneno muhimu ili kuwasaidia walengwa wasiyasahau².

Dhana ya balagha imefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Mathalani, TUKI (2013) inafasili kuwa balagha ni ustadi wa kutumia lugha ili kushawishi au kufurahisha. Pia, JKF (2016) inafasili kuwa balagha ni usemaji mahiri, kwa mfano, ameshinda kiti cha ubunge kwa sababu yeye ana balagha. Nao Richard na wenzake (1992) wanafasili balagha kuwa ni stadi ya mtindo wa lugha kupitia uchambuzi wa kisarufi na kimantiki. Wakifafanua zaidi, wanaeleza kuwa kwa kutumia balagha wanasiasa huipamba lugha kwa tamathali za semi, vionjo mbalimbali vya lugha na mitindo anuwai ya matumizi. Kwa muktadha huu, ni dhahiri kwamba ustadi au kipaji cha kutumia lugha hutegemeana na kilongo cha mazungumzo. Katika uchunguzi huu, tunachukulia kuwa balagha ni matumizi ya lugha kwa ustadi na umahiri mkubwa yenye lengo la kushawishi na kuhamasisha ili kufikia azma iliyokusudiwa na kukubalika. Hata hivyo, Nadharia ya Balagha imetoa indhari kwamba si lazima kila jambo liweze kumshawishi kila mtu kwa kiwango sawa (Lupogo na Ambrosi, 2023). Hivyo, wazungumzaji weledi hujinoa katika mbinu za kibalagha zenye kuleta mvuto masikioni mwa hadhira. Jambo hili pia linaungwa mkono na Mwansoko (1994) anayefafanua kuwa lugha inayotumiwa kwenye shughuli za kisiasa kwa ujumla wake huwa ni ya kuvutia sana. Lugha hiyo hupambwa vizuri ili kumfanya msikilizaji awe na ari, mvuto na ajisikie kuibua hisia fulani. Hisia hizo zinaweza kuwa za furaha, huzuni, masikitiko, chuki na kadhalika. Hivyo, dhana za kiisimu zinazotumika hapo, hasa msamiati au tamathali za semi kama sitiari, tasifida, tashibiha husaidia sana kuleta msimko katika mawasiliano ya mtindo huu wa kisiasa. Si kitu cha ajabu kwa wazungumzaji kuzitumia tamathali za kibalagha kuongezea utamu na kuleta athari chanya kwa hadhira. Uchunguzi huu umebaini kuwa kuna ujitokezaji wa matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya umoja na wingi, tafsida, misemo, vitambulisho hadhi, takriri, ufutuhi, masimulizi ya hadithi na kuchanganya msimbo katika hotuba mbalimbali za Samia. Kwa ujumla, matumizi ya mbinu hizo husaidia kufikisha ujumbe kuhusu uwajibikaji, kuonesha

² Katika <https://www.coursehero.com>

mshikamano, kutoa matumaini, kulinda utu wa watu, kusisitiza juu ya masuala mbalimbali, kuhimza maendeleo na kuonesha falsafa yake ya kiuongozi kwa wananchi.

2.0 Mkabala wa Kinadharia

Utafiti uliozaa makala haya umeongozwa na Nadharia ya Balagha ambayo chimbuko lake lilianzia kwa Aristotle mwaka 367 KK. Neno balagha ni kisawe cha neno la Kigiriki *rhetor* likiwa na maana ya namna ya kuwa msemaji bora. Kwa maelezo ya Zheng (2014), Aristotle alitazama balagha kama nyenzo ya kuvumbulia njia mbalimbali za kushawishi umma katika mada yoyote ile inayohusiana na jambo linalowasilishwa. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), Nadharia ya Balagha ina chimbuko lake katika jadi ya Kiyunani na Kirumi ambapo ilianguziwa katika makundi matatu makuu: mosi, balagha ya kisheria/kilengo; pili, balagha ya kiutetezi/kihukumu, na tatu ni balagha ya kiushawishi/kisifa/kisherehe. Nadharia ya Balagha ilipata umaarufu mkubwa na maendeleo yake katika kipindi cha miaka 2000. Wachunguzi wa Kirumi, Cicero na Quintilian, kama walivyonyukuliwa na Ward (1995), walirejelea kazi ya Aristotle ambapo wanafunzi wengi wa vyuo vikuu walihitaji kujifunza sanaa ya balagha katika kipindi cha karne ya 18 na 19. Hivyo basi, balagha kama nadharia ni nadharia ya uchunguzi wa lugha ambayo hujikita katika maneno ya ushawishi kuhusu mada inayowasilishwa mbele ya hadhira lengwa.

Katika muktadha huo, Nadharia ya Balagha imejikita katika kuelezea kinagaubaga jinsi ya kujenga ushawishi wa jambo lolote linalowasilishwa mbele ya hadhira lengwa. Kwa hiyo, katika nadharia hii kuna mbinu ambazo msemaji anatakiwa kuzitumia ili anachokiwasilisha kiushawishi hadhira aliyoilenga (Lupogo na Ambrosi, 2023). Hivyo, uchunguzi huu ulilenga kubainisha mbinu hizo kama zinavyojitokeza katika hotuba mbalimbali za Samia.

2.1 Mihimili ya Nadharia ya Balagha

Nadharia ya Balagha imejengwa katika mihimili mikuu mitatu, yaani mhimili wa yaliyomo katika usemi, mhimili wa mtindo na mhimili wa mpangilio wa hotuba au usemi. Mihimili hiyo imefafanuliwa kama ifuatavyo:

2.1.1 Mhimili wa Yaliyomo katika Usemi

Katika mhimili huu Aristotle ana maana kwamba katika kumchunguza msemaji au usemi, mtafiti hana budi kumakinikia viwango vitatu ambavyo ni kiwango cha Logosi, Pasosi na Esosi kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

- a) Kiwango cha Logosi: katika kiwango hiki Aristotle anahimiza kuwa mtafiti azingatie namna msemaji anavyoweza kuibua hoja au maswali yenye kumpa msikilizaji muda wa kutafakari badala ya kujibu (mbinu ya kuuliza maswali isiyohitaji majibu).

- b) Kiwango cha Pasosi: Aristotle katika kiwango hiki anahimiza mtafiti atathmini hisia za wapokeaji wa usemi kulingana na uzito wa hoja zilizomo katika usemi huo.
- c) Kiwango cha Esosi: Aristotle anatoa ufafanuzi kuwa wapo wazungumzaji wenye sifa na tabia zinazowafanya waheshimiwe, wenziwe na kukubaliwa kabla na baada ya usemi wao kwa hadhira. Hivyo, ni vyema mtafiti kuzingatia sifa bainifu zifuatazo: uwezo wa jambo analolizungumzia msemaji, namna anavyolichukulia suala analolizungumzia na ubinadamu alionao mzungumzaji kwa hadhira. Kwa hivyo, ukubalifu na uaminifu wa msemaji kwa hadhira ni jambo la msingi sana.

2.1.2 Mhimili wa Mtindo

Katika mhimili huu, Aristotle anasisitiza kwamba mtafiti ajikite katika kuchunguza namna ambavyo mbinu za kifani zinasababisha hotuba au usemi kuwa na ushawishi mkubwa kwa hadhira. Mhimili huu ulisaidia sana katika kuchambua mbinu mbalimbali za kibalagha ambazo zimejitokeza katika hotuba za Samia na namna zilivyochangia kushawishi hadhira.

2.1.3 Mhimili wa Mpangilio wa Hotuba au Usemi

Aristotle, katika mhimili huu, anahimiza suala la mpangilio wa hotuba. Mtafiti azingatie mwanzo au utangulizi (jinsi ambavyo mzungumzaji alivyoanza hotuba au usemi wake kwa hadhira), kiini cha usemi huo (jinsi mzungumzaji alivyojenga hoja na kuendeleza hoja zake) na kisha achunguze vile alivyohitimisha hoja katika usemi wake. Kwa ujumla, ukichunguza mihimili hii yote mitatu unabaini kwamba inakwenda sambamba katika utendaji kazi wake. Katika uchunguzi huu, takribani mihimili yote imetumiwa katika kubaini mbinu za kibalagha zilizotumiwa na Samia katika hotuba zake.

Kwa kutumia mkabala huu, imebainika kwamba Samia kama mwanasiasa hutumia mbinu mbalimbali za kibalagha katika kushawishi na kuvutia hadhira yake. Samia huteua mitindo mbalimbali ya lugha ili kuhakikisha anashawishi na kuamsha ari.

Aidha, kwa kutumia Nadharia ya Balagha, imedhihirika kwamba Samia hutumia vipengele anuwai vya ushawishi na msukumo wa mawasiliano unaomfanya akubalike kwa hadhira na kuchota fikra zao juu ya mambo ya kiutekelezaji aliyoyakusudia. Maelezo kuhusu utendaji wa balagha yanafafanuliwa pia na Nokkonen (2007) ambaye anaeleza kwamba tunapobainisha kwa ujumla nini hasa kinafanyika katika uchanganuzi wa kibalagha wa kilongo au hotuba tunajiweka katika nafasi ya kuchunguza kwa namna gani msemaji au mwandishi anatushawishi kupitia mambo yafuatayo:

- a) Namna msemaji/mwandishi anavyoshawishi au kuhamasisha hadhira fulani katika mazingira fulani.
- b) Njia au mbinu zipi amezitumia katika kuihamasisha hadhira.
- c) Je, hoja zina mantiki ipi?

- d) Ni aina gani ya msamiati, misemo au sitiari alizozitumia?
- e) Ni nafasi gani ambayo wasemaji/waandishi wamejichukulia na wanamilikishwa vipi nafasi hizo? Kwa ujumla, uchanganuzi kwa kutumia Nadharia ya Balagha umetoa fursa ya kubaini na kuchambua mbinu za kibalagha na kuchunguza dhima ya mbinu hizo.

3.0 Methodolojia

Data za msingi za utafiti uliozaa makala haya zilikusanywa kwa mbinu ya ushuhudiaji na usikilizaji wa hotuba. Hotuba mbalimbali za Samia zilipakuliwa kutoka katika mtandao wa kuhifadhi video wa *YouTube*. Mbinu ya ushuhudiaji pia ilitumika kwa mwandishi kushiriki moja moja katika kusikiliza na kufuatilia hotuba hizo. Kwa pamoja, mbinu ya ushuhudiaji na usikilizaji wa hotuba zilisaidia kupata data zote za msingi. Kupitia mbinu hizi tulipata kauli mbalimbali zilizojitokeza katika hotuba zake mbalimbali.

Data hizo zilirekodiwa na kunukuliwa katika maandishi na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Makala haya yamegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili inahusu mkabala wa kinadharia uliotumika katika uchambuzi wa data za makala haya, sehemu ya tatu inafafanua methodolojia iliyotumika kubainisha mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data. Aidha, sehemu ya nne ambayo ndiyo kiini cha makala haya, imejikita kubainisha mbinu za kibalagha zilizojitokeza katika hotuba za Samia na sehemu ya tano inatoa hitimisho la mjadala wa makala haya.

4.0 Ujitokezaji wa Mbinu za Kibalagha katika Hotuba za Samia

Sehemu hii inadhihirisha matokeo ya matumizi ya mbinu za kibalagha katika hotuba za Samia.

4.1 Matumizi ya Viwakilishi vya Nafsi za Umoja na Wingi

Viwakilishi vya nafsi ni maneno yanayosimama badala ya majina ya watu (BAKITA, 2016). Mfano viwakilishi vya nafsi katika Kiswahili ni *mimi* (nafsi ya kwanza umoja), *sisi* (nafsi ya kwanza wingi), *wewe* (nafsi ya pili umoja) na *nyinyi* (nafsi ya pili wingi), *yeye* (nafsi ya tatu umoja) na *wao* (nafsi ya tatu wingi). Baada ya kutoa ufafanuzi kuhusiana na dhana ya nafsi, tunaweza kusema kuwa nafsi ni kipengele kinachomdhihirisha mhusika katika usemaji. Matokeo ya utafiti uliozaa makala haya yamebainisha kuwa Samia hutumia viwakilishi mbalimbali vya nafsi, umoja na wingi, kama mbinu ya kibalagha kuonesha upamoja na utayari wake wa kuitumikia taifa. Dondoo namba 1 linadhihirisha hapa chini:

- 1) ...Ninalotaka kuwaambia ndugu zangu na wananchi, **nitajitahidi ninavyoweza**, kila fursa **nitakayoiona itakayoletwa** kutoka duniani ambayo **naweza kuitumia kuleta maendeleo Tanzania nitaitumia**,

na **ninafanya** hivi **ninafanya** hivi kwamba **niliapa** kwa Mungu **nitaitumikia** Tanzania wala sifanyi hivi kwa uchaguzi wa 2025...

Chanzo: Hotuba ya SSH aliyoitoea Ikulu-Dar es Salaam, 4 Januari 2022

Pia, matumizi ya viwakilishi vya nafsi tunaweza kuviona katika dondoo namba 2:

- 2) ...Mheshimiwa Spika sasa naomba **mniruhusu** nitaje baadhi ya masuala muhimu ambayo serikali ya awamu ya sita itayapa kipaumbele kwenye miaka mitano hii. Jambo la kwanza na la muhimu kabisa **tutakalolipa** kipaumbele kwenye miaka hii mitano ni kuendelea kulinda na kudumisha tunu za taifa **letu** (makofi) yaani, amani, umoja na mshikamano, uhuru wa nchi **yetu**, Mapinduzi matukufu ya Zanzibar pamoja na muungano **wetu**. (makofi)

Chanzo: Hotuba ya SSH aliyoitoea Bungeni-Dodoma, 22 Aprili 2021

Katika mfano wa (1) na (2) hapo juu, tunabaini kuwa Samia anatumia viwakilishi vya nafsi ya kwanza umoja **ni** na nafsi ya pili wingi **tu**. Mfano katika maneno **nitajitahidi**, **ninavyoweza** na **tutakalolipa**, **yetu**, **wetu**. Viwakilishi hivyo hutumika kuonesha ustadi wa lugha katika kuleta ushawishi kwa hadhira juu ya mada inayowasilishwa.

Matumizi ya viwakilishi hivi vya umoja yanadhihirisha nia yake ya dhati ya kulitumikia taifa la Tanzania. Katika maelezo hayo, angeweza kujitaja kwa jina, lakini anatumia kiwakilishi cha nafsi kama kibainishi cha mbinu ya kibalagha kuishawishi hadhira ili imwamini juu ya mambo ambayo anaahidi kuyafanya kwa jamii ya Watanzania. Vilevile, katika mfano wa (2) ametumia viwakilishi vya nafsi ya kwanza wingi ambavyo vinadhihirisha kuwa Samia katika uendeshaji wa serikali atashirikiana na viongozi wenzake. Kwa mfano, pale anaposema “Jambo la kwanza na la muhimu kabisa **tutakalolipa** kipaumbele ni...” hii inadhihirisha kuwa matumizi ya mbinu hii yanabainisha kuwa Samia ni mtu mwenye kupenda ushirikiano na mshikamano katika kuendesha serikali. Angeweza kutumia nafsi ya umoja kujirejelea mwenyewe lakini hakufanya hivyo kwa sababu alikusudia kushirikiana na wenzake. Kwa kutumia mbinu hii ya kiushawishi, wasikilizaji ambao ni viongozi wenzake hufurahi na kujiona wao pia ni sehemu ya uongozi wa awamu yake. Licha ya kuwa Samia ndiye Rais na mwenye mamlaka makubwa kuliko viongozi wengine, bado katika matumizi yake ya lugha anatumia mbinu hii. Kwa hakika, anatumia viwakilishi vya nafsi ya kwanza wingi ili kuonesha kuwa uamuzi atakaoufanya sio wa kwake pekee bali utawahusu viongozi wote.

4.2 Tasifida/Mafumbo

Tasifida ni utumiaji wa maneno, misemo au nahau ambazo hupunguza ukali au matusi yaliyomo kwenye maneno hayo (Senkoro, 2008). Uchunguzi katika makala haya umebaini kuwa Samia katika hotuba zake hupenda sana kutumia lugha ya tasifida na yenye mafumbo kwa kiasi fulani. Mfano ufuatao unadhihirisha hilo:

- 3) ...Na hapa inanikumbusha hadithi moja, kuna mtu mmoja ‘**wiseman**’ wa makamo, nilipotwishwa huu mzigo alinitafuta, aliponipata akanambia mama nimekuja kukupa hongera lakini pole. Nikamwambia napokea. Akanipa mawaidha mengi akanambia lakini nataka nikwambie, atakayekusumbua kwenye kazi yako na uongozi wako ni **shati ya kijani mwenzio** wala si mpinzani, huyo ndiye atakayekusumbua. Mpinzani atakutazama unafanya nini, ukimaliza hoja zao hawana maneno lakini **shati ya kijani mwenzio** anayetazama mbele mwaka 2025, 2030 huyo ndiye atakayekusumbua. Nataka niwaambie ndicho kinachotokea, ndicho kinachotokea. Fikiria mtu niliemuamini, mshika muhimili aende asimame aseme yale bila shaka hii ni **stress** ya 2025...

Chanzo: Hotuba ya SSH aliyoitoea Ikulu-Dar es Salaam, 4 Januari 2022

Matumizi ya tasifida pia yanajitokeza katika dondoo namba 4 kama ifuatavyo hapa chini:

- 4) ...Nilitegemea kwamba yeye ndio atakuwa na uelewa na hasa kwa sababu mabajeti yote, (ma)mikopo yote, taarifa zote za kiuchumi ndani ya **nyumba yake** wasameheni...

Chanzo: Hotuba ya SSH aliyoitoea Ikulu-Dar es Salaam, 4 Januari 2022

Katika mfano wa (3) hapo juu, tunabaini kuwa Samia anatumia tafsida inayosema, **shati ya kijani**. Ingawa maneno hayo ni maarufu kwa jamii lakini ametumia lugha ya tasifida kuonesha staha kwa mtu aliyekua anamrejelea. Taswira inayojengwa na kuzingatia muktadha wa mazungumzo ‘shati la kijani’ wanaozungumziwa ni wanachama wenzake wa CCM. Samia hakuwataja moja kwa moja ila ametumia mbinu ya tasifida kuwarejelea watu hao. Hii ni kwa sababu wanachama wa CCM wana sare yao ya chama ambayo ni ya rangi ya kijani. Kuonesha umahiri wa lugha na kuchunga staha ya hadhira, anatumia tasifida ya **shati ya kijani**. Kufikisha ujumbe aliokusudia kwa jamii.

Ama katika mfano wa (4) inaelekea mazungumzo yake yalikuwa yakimhusu mtendaji mmoja mkubwa wa mhimili katika mihimili ya nchi. Hakumtaja waziwazi bali alitumia mbinu ya kibalagha ya tasifida kwa kufikisha ujumbe wake. Mfano, aliposema ‘mambo hayo yanapitia katika **nyumba yake** ...’ kinachorejelewa hapa si

nyumba ya huyo mhusika bali ni chombo au mhimili anaousimamia. Kadhalika, akatumia balagha ya taswira ya mbali kwa kuutaja mwaka *twenty twenty-five fever*, akimaanisha ‘homa ya mwaka 2020 – 2025’ (maandalizi ya uchaguzi mkuu). Taswira inayojengwa hapo ni ya kinyang’anyiro cha uchaguzi wa mwaka 2025 na si kingine. Kwa kawaida, katika kuelekea kwenye chaguzi kuu kuna masuala mbalimbali hujitokeza. Hivyo, hakuamua kurejelea dhana hizo moja kwa moja ila alitumia lugha ya mafumbo kufikisha ujumbe wake aliokusudia.

4.3 Matumizi ya Misemo na Hekima ya Lugha za Kigeni

Maneno ya hekima ni semi ambazo hutumiwa na wanajamii kwa namna maalumu ili kulinda maadili ya jamii. Wanasiasa nao hutumia misemo ya hekima ya wahenga katika hotuba zao ili kuhakikisha kuwa wamefikia malengo yao (Man, 1984). Samia naye kama mwanasiasa na mwanajamii, tumebaini kuwa hutumia mbinu ya misemo ya aina mbalimbali kama vile misemo ya kawaida, misemo ya hekima ya lugha za kigeni na misemo ya vijana katika hotuba zake.

4.3.1 Matumizi ya Misemo

Hii ni aina ya misemo ambayo hutumika katika muktadha wa kawaida. Tuangalie dondoo lifuatalo:

- 5) ...Fanyeni kazi kwa lengo moja kwamba tunawatumikia Watanzania, sisi ni watumishi wa Watanzania, na nitakuwa na kipimo cha mabega, nikiona mtu **mabega yanazidi kupanda juu**, nitajua huyu sio mtumishi, huyo *anaenjoy* juu ya kiti chake na ni jambo ambalo silitarajii, natarajia mawaziri nisikie mko huko na huko mkiwatumikia Watanzania

Chanzo: Hotuba ya SSH aliyoitoa Ikulu-Dodoma, 1 Aprili 2021

Katika mfano wa 5 hapo juu tunabaini kuwa Samia hutumia misemo ya kawaida katika hotuba zake. Kwa mfano, *kuinua mabega* ni msembo ambao hutumika kurejelea tabia ya kujidai, kujisikia na kujiona bora kuliko watu wengine. Katika madondoo hayo, Samia anaonesha umbuji wa matumizi ya lugha kwa kutumia msembo mwingine wa *kuenjoy*, yaani ‘kula raha na starehe’. Mbinu hii ya misemo inakwenda sanjari na ujumbe aliokusudia wa kuwataka viongozi wateuliwa wasiwe na tabia za kujidai, kujisikia na kuendekeza starehe tu. Badala yake wajikite katika kutatua shida na changamoto zinazowakabili Watanzania. Kuonesha umbuji na umahiri wa lugha zaidi anawaambia, ‘sitarajii tabia kama hizo’. Hapa anamaanisha kwamba ikiwa kuna baadhi ya viongozi wenye kuwaza hayo waache. Katika jamii, baadhi ya viongozi wanapopata madaraka hujikuta wakianza kujidai, kujisikia na kuendekeza starehe. Kwa kutumia mbinu hii ya kiushawishi ya msembo huu, Samia anawakumbusha na kuwaonya viongozi husika kuwa hatarajii hayo anayoyatolea angalizo yakitokea.

4.3.1 Misemo ya Hekima ya Lugha za Kigeni

Katika hotuba zake, Samia ameonesha kuwa ni mlumbi na mbuti wa lugha. Hayo yanabainishwa na matumizi ya mbinu ya misemo ya hekima ya lugha ya Kiarabu na Kiingereza. Samia hutumia misemo hii kutaka kuonya, kuelekeza au kufundisha hadhira juu ya jambo fulani. Tazama dondoo namba 6 linalodhihirisha hali hiyo:

- 6) ...kama ulipata malezi mazuri, ukajua dini yako, ukakua kwenye misingi mizuri kuna mambo huwezi kufanya. Kwa hiyo mengine yanayotokea unamtazama mtu unasema aaah!! ***Fungu la Arham, Al jununu fununu*** sasa utasikia ooh!! Mama ana kifua, unastahamili, unafanyaje sasa! Kama mwendawazimu anachukua nguo zako anakwenda mbio anatoka utupu umfukuze mwendawazimu ni yupi? Wengine tulilelewa kwenye maadili na tukapitishwa kwenye dini na tukazielewa dini zetu vizuri hatuwezi kufanya hayo...

Chanzo: Hotuba ya SSH aliyoitoa Ikulu-Dar es Salaam, 3 Januari 2023

Aidha, hali ya matumizi ya misemo ya hekima ya lugha ya kigeni yanabainika katika dondoo namba 7 kama ifuatavyo:

- 7) ...Huko nyuma wazee wetu walitambua, **argue, don't shout**, yaani lumbana kwa hoja lakini usipige makelele, zungumza kwa hoja...

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Matembezi ya UVCCM ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, 10 Januari 2024

Katika mfano wa 6 hapo juu, tunabaini kuwa Samia anatumia mbinu ya misemo yenye maneno ya Kiarabu kama vile ***'fungu la arhamu'*** na ***'aljununu fununu'***. Msemo ***fungu la arhamu*** unamaanisha 'fungu au kundi la kuonewa huruma', yaani la kurehemiwa na msemo ***aljununu fununu*** una maana ya: *jununu* = mtu kichaa, mwehu; na *fununu* = fani, yaani, ukichaa upo wa aina/fani nyingi. Kuna mwingine ukichaa wake ni kutukana, mwingine ukichaa wake ni kupiga kelele, mwingine kupenda fujo na purukushani n.k. Samia anatumia mbinu hii ya kibalagha kuwasema baadhi ya viongozi ambao wanapenda fujo na purukushani kila wakati, wanaotamka maneno yasiyo ya staha na ya kuleta fujo tu kwa kuwa tu wanadai jambo fulani. Samia angaliweza kutamka maneno hayo kwa lugha ya wazi tu na kwa ukali, lakini anaonesha umbuji na ubalagha kuishawishi/kueleza jamii. Kwa kutumia misemo hiyo ya lugha ya Kiarabu, Samia anafikisha ujumbe kuwa 'watu hao ni fungu la kusamehewa tu maana kila mtu ana ukichaa wake'.

Aidha, katika mfano wa 7 tunabaini kuwa Samia anatumia msemo wa *argue don't shout* akiufafanua kuwa maana yake ni 'hoji usipige makelele'. Samia anatumia mbinu hii kulikumbusha na kulielimisha kundi la vijana anaowahotubia. Anawaelimisha kuwa wawe na tabia ya kujenga hoja na si kubishana tu bila ya kuwa na hoja katika mambo anuwai yanayohusu nchi. Vijana wawe na tabia ya kulumbana kwa hoja na si kwa kufanya kelele tu. Samia angeweza kutumia lugha nyingine yoyote ile ila anawakumbusha kwa kutumia msemo huo ambapo anasisitiza kuwa hata yeye alifundishwa hivyo na wazee.

4.3.2 Misemo ya Vijana

Uchunguzi katika makala haya umebaini kuwa Samia ni mwanamarika (hotuba zake zinaendana na umri wa hadhira). Katika hotuba zake mbalimbali imebainika kuwa hutumia mbinu ya misemo inayozingatia marika mbalimbali likiwamo rika la vijana. Tazama dondoo lifuatalo:

- 8) ...Wewe ni kijana, mimi ni mama. Ukinizingua tutazinguana (*kicheko*) nataka ukafanye kazi...

Chanzo: Hotuba ya SSH aliyoitoa Ikulu-Dodoma, 6 Aprili 2021

Hali ya Samia kutumia misemo kwa kuzingatia rika la hadhira anayoihutubia, pia tunaweza kuona katika dondoo namba 9 hapa chini:

- 9) ...Twendeni tukafanye siasa za kistaarabu, tusiende kutukanana, sio mila zetu, kusimama jukwaani 'Wewe Samia Suluhu wewe hauna adabu wewe, miguu yako imekwenda upande wewe kichwa kama mbuzi', Samia Suluhu anaweza akawa na upeo mzuri wa ustahamilivu kama alionao kwa sababu yananiyata ila nanyamaza lakini Mshabiki wa Samia, **chawa wake** anaweza asistahamili akaja akavaana na **chawa wako** wewe uliyetukana balaa likianza hapo kwa hiyo tusiende kuchokozana".

Chanzo: Hotuba ya SSH aliyoitoa Ikulu-Dar es Salaam, 3 Januari 2023

Katika madondoo namba 8 na 9 tunabaini kuwa Samia ametumia misemo *ukinizingua, tutazinguana* na msimu *chawa* ambayo aghalabu hutumiwa na vijana katika miktadha yao. Neno 'zingua' lina maana ya 'kubabaisha mtu'. Vijana hutumia neno hilo wanapotangamana na vijana wenzao hasa wasipotaka kubabaishwa juu ya jambo fulani. Samia kwa kutumia mbinu hii ya kibalagha anatumia neno mwafaka linalokwenda sanjari na mhusika kijana ambaye ni kiongozi aliyemteua na hata na vijana wengine. Anataka ujumbe wake ufike pengine bila kumkwaza mhusika. Hivyo, anatumia msemo huu kama mbinu ya kibalagha kumweleza kuwa katika majukumu aliyopewa, ikiwa atababaisha basi na yeye atambabaisha. Pia, katika neno *chawa* ambalo kimsingi humaanisha 'mdudu

anayependa kukaa sehemu yenye uchafu'; matumizi ya neno hilo katika rika la vijana hayana maana hiyo kabisa. Vijana wanapotumia neno 'chawa' humaanisha 'mpambe, mtu wa karibu na mtu fulani mwenye uwezo wa fedha au cheo cha juu au mfuasi wa mtu tajiri'. Samia anatumia mbinu ya msimu *chawa* kuwakumbusha wadau wa siasa aliokuwa akiwahotubia kuwa watumie lugha nzuri na yenye staha katika mikutano yao. Kwani kama watatukana basi *chawa* wake, yaani mpambe, akereketwa, wafuasi wake nao hawatakubali, matokeo yake kutakuwa na vurugu na hali ya amani kutoweka. Hivyo, matumizi ya msemo huu yamesaidia sana katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa hususani kwa viongozi wote ambao ni vijana.

4.4 Vitambulisho Hadhi

Sylvester (2015) anafafanua kuwa haya ni maneno yenye lengo la kuonesha utii, heshima, urafiki na ukubalifu wa kijamii. Kwa hivyo, maneno haya ni muhimu katika kulinda staha. Mathews (1997) anaeleza kuwa vitambulisho hadhi ni namna mojawapo ya viwakilishi au vitenzi vinavyotumika kuonesha heshima kwa mtu fulani, mathalani, mtu mwenye hadhi ya juu ya kijamii. Kwa mujibu wa Huang (2008) na Habwe (2010), kitambulisho hadhi lazima kioneshe heshima na staha kwa anayehusika. Habwe anaongeza kuwa utambulisho hadhi haulengi kulinda staha kwa mhusika tu bali pia kwa jamii. Hii ni sawa kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Balagha kwenye mhimili wa pili katika kiwango cha Esosi, ambapo Aristotle anatoa ufafanuzi kuwa wapo wazungumzaji wenye sifa na tabia zinazowafanya waheshimiwe, kuenziwa na kukubaliwa kabla na baada ya usemi wao kwa hadhira. Kwa kulizingatia hilo, imebainika kuwa Samia amekuwa akitumia sana mbinu hii ya vitambulisho hadhi ili kulinda staha na heshima za wahusika na jamii kwa ujumla. Hebu tuchunguze dondoo lifuatalo:

- 10) ...Leo tunaandika historia mpya katika jitihada za kuendeleza kuimarisha Taifa letu, niwapongeze wanaume waliopo hapa ndani, mnajua peke yetu wanawake hatuwezi, lazima wanaume muwepo. Nimefurahi namuona **mwanangu Wenje** yupo hapa kanawiri, na **mwanangu Lema** yupo hapa karibuni Tanzania hii ndio Tanzania njema...

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Kongamano la Wanawake wa CHADEMA-Moshi, 8 Machi 2023

Pia, matumizi ya vitambulisho hadhi katika hotuba za Samia tunayabaini katika dondoo la 11 hapa chini:

- 11) ...Ndugu zangu na hasa Askofu Shoo, **kaka yangu Askofu Mkuu** wa Kanisa...Nimeyasikia yote

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Hafla ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Kanisa la KKT Makumira-Arusha, 21 Agosti 2023

Aidha, hali ya matumizi ya vitambulisho hadhi katika hotuba za Samia yanadhihirika katika dondoo la 12 kama ifuatavyo:

- 12) ...Niwapongeze **wanangu wa Yanga na Simba** kwa kutumia vizuri fursa niliyowapa ya goli moja Milioni tano wametumia vizuri sana. Kwa hesabu nilizo nazo nadhani Yanga wameishalamba Milioni 30 na Simba jana Milioni 35 kwa hiyo niwapongeze kwa kutumia fursa hii...

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Sherehe za Kilele cha Miaka Miwili ya Uongozi wake Uwanja wa Uhuru-Dar es Salaam, 19 Machi 2023

Katika madondoo ya (10), (11) na (12) tunaona kuwa Samia ametumia vitambulisho hadhi mbalimbali katika hotuba zake. Matumizi ya mbinu hii ya vitambulisho hadhi kama vile pale anaposema: *mwanangu Wenje, mwanangu Lema, Ndugu zangu, Kaka yangu Baba Askofu na wanangu wa Yanga na Simba*, yanaonesha moja kwa moja kuwa vinalinda staha na heshima ya wahusika na jamii kwa ujumla. Samia kwa makamu yake, kuwarejelea viongozi wa CHADEMA kama vile *mwanangu Wenje* na *mwanangu Lema* ambao walikuwa wabunge miaka iliyopita waliokwenda kuishi nje ya nchi kutokana na changamoto za kisiasa. Samia anatumia mbinu hii ya kiushawishi ya vitambulisho hadhi vya *wanangu* akiwachukulia kuwa kama watoto wake wa kuwazaa na hivyo wanastahili heshima na kuwajali kama wanawe. Vivyo hivyo, kwa Askofu Shoo, licha ya kumtambua kwa hadhi yake ya uaskofu, bado amemrejelea kama *kaka yake*. *Kaka* kwa dhati ya lugha ni ndugu mkubwa wa kiume unayezaliwa naye. Samia anatumia mbinu hii ya kibalagha kwa kutumia kitambulisho ‘kaka’ kwa Askofu Dkt. Shoo kama njia ya kistaha na ya kiushawishi ya kutambua hadhi yake katika jamii. Vilevile, katika mfano 12 tumeona wachezaji wa Yanga na Simba wote akiwarejelea kama wanangu.

4.5 Matumizi ya Takriri

Takriri ni matumizi ya lugha yanayoonesha kitendo cha msemaji kurudiarudia maneno, sauti, wazo au vifungu fulani katika kazi yake. Watunzi hutumia takriri ili kutia uzito maneno yanayorudiwarudiwa au kuweka msisitizo ili msomaji aweze kupata ujumbe uliokusudiwa na mtunzi (Ntarangwi, 2004; Wamitila, 2008). Hali kama hii ya kurudiarudia maneno haibainiki katika kazi za kifasihi tu, bali hata viongozi wa kisiasa hutumia takriri wanapokuwa wakitoa hotuba zao. Katika makala haya tumbaini kuwa Samia hutumia mbinu hii kwa kufanya takriri katika hotuba zake. Tazama dondoo lifuatalo:

- 13) ...Niliamua kunyamanza kimya na ninaendelea kunyamanza kimya..(makofi) Ninachotaka kuwahakikishia,

Hakuna mwenye misuli na ubavu wa kuligawa taifa hili, (makofi)

Hakuna mwenye misuli na ubavu wa kuuza taifa hili,

Hakuna mwenye misuli na ubavu wa kuharibu amani na usalama tulioujenga kwenye taifa hili...

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Hafla ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Kanisa la KKT Makumira-Arusha, 21 Agosti 2023

Katika dondoo la 13 hapo juu tunaona kuwa Samia ametumia mbinu ya takriri ya maneno *hakuna mwenye misuli na ubavu* wa kuligawa taifa, wa kuuza taifa na wala wa kuharibu amani na usalama wa taifa la Tanzania. Urudiaji wa maneno hayo unajenga hisia ya uhakika na msisitizo wa uimara kuwa hakuna mtu wa aina yoyote anayeweza kusambaratisha taifa. Mukstadha wa wakati alipotoa hotuba hiyo, ilikuwa ni katika kipindi ambacho nchini Tanzania kulikuwa na mjadala mrefu na mpana kuhusu uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam na Kampuni ya DP World. Baadhi ya maoni katika mijadala hiyo hayakuwa na lugha ya staha na yalionesha kutaka kuvuruga na kuvunja amani na usalama wa nchi. Samia kama mlumbi wa lugha alitumia mbinu ya kibalagha ya takriri kwa kusimika kauli hiyo na kuonesha msisitizo kuwa hao wanaojadili wasidhani kuna mtu mwenye misuli wa kuliteteresha taifa.

4.6 Matumizi ya Ufutuhi

Kwa mujibu wa Ponera (2014), ufutuhi ni mbinu ijengwayo na maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye mnato na mvuto hadi kuwafanya watu wachangamke, wafurahi na watabasamu au wacheke. Fasili hii ya Ponera inajumuisha mambo matatu kwa pamoja, yaani ucheshi, vicheko na furaha. Sovu (2020) anasema kuwa kuna namna ambayo mbinu ya usimuliaji katika hotuba za wanasiyasa na hata matendo yao huifanya hadhira kucheka au kutamani kucheka. Kicheko hicho huibuliwa na sifa ya vitu, hali, lugha au mazingira. Samia kama mwanasiyasa katika hotuba zake hutumia mbinu za kibalagha zenye kudokeza ucheshi, utani au furaha fulani. Chunguza dondoo hapa cha chini:

14) ...Habari za mchana, juzi Ruto alitufundisha jambo! Akasema semeni jambo lakini the *real thing* ni habari za mchana (makofi).

Hawa Wakenya hawa kwenda kusaini mkataba, wanasema kuweka kidole (vicheko) inabidi tuwaweke kwenye *lesson* za Kiswahili...

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Mkutano wa Jukwaa la Chakula jijini Dar es Salaam, 8 Septemba 2023

Vilevile, hali ya matumizi ya ufutuhi katika hotuba za Samia inabainika katika dondoo la 15 kama ifuatavyo:

- 15) ...Kule Zanzibar kuna mshairi aliimba, nyumba uliyoizoea kuihama ina tabu, **ni kazi kwelikweli kuhama nyumba uliyoizoea na wanaume wanajua hilo** (vicheko na shangwee) CCM hoyee, (hoyee) wameshindwa kuimba wimbo wa bwana ugenini, si ndio sasa tuwakaribishe nyumbani tuje tuimbe nao ndani ya nyumba...

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM-Dodoma, 30 Aprili 2023

Katika dondoo la 14 tumebaini kuwa Samia ametumia lugha ya ucheshi kwa kurejelea matumizi ya Kiswahili cha majirani zake Wakenya. Matumizi ya mbinu hii ya kifutuhi, yanakuwa katika hali ya ucheshi na kufurahisha kama mbinu ya kibalagha lakini hubeba ujumbe fulani. Maelezo haya, ingawa yanasisitiza umuhimu wa Wakenya kujifunza Kiswahili sanifu na fasaha zaidi, yamejaa staha kiasi kwamba wasikilizaji wanapata furaha tu bila kuhisi vibaya.

Ama katika dondoo la 15 tunaona kuwa Samia anarejelea kipande cha wimbo wa taarabu asili ya Zanzibar uitwao “Dunia Ina Fisadi”. Ucheshi huo ulilenga kumpokea ndugu Lazaro Samueli Nyalandu aliyekuwa akirejea kujiunga na Chama cha Mapinduzi. Hapo ndipo Samia alipompokea na kumkaribisha nyumbani (CCM) kwa kusema nyumba *uliyoizoea kuihama ina kazi na wanaume wanajua*. Hadhira ilitabasamu na kufurahi kwa kurejelea namna alivyorudi nyumbani.

4.7 Masimulizi ya Hadithi/Michapo

Kwa mujibu wa BAKITA (2016), mchapo ni masimulizi au hadithi ya tukio fulani ambayo yametiwa chumvi mno ilimradi yasisimue. Mulokozi (2017) anaeleza kuwa masimulizi ni fasihi ya kifani ambayo huwa na sifa za mpangilio fulani mahususi, huwa na wahusika, yaani watendaji katika matukio yanayosimuliwa, hutumia lugha ya kimaelezo, utambaji wake huambatana na vitendo au ishara, na huwa na maudhui ya kweli au ya kubuni na yenye mafunzo fulani katika jamii. Hadithi ni masimulizi kuhusu matukio yaliyopita, yaani habari, visa au hekaya (BAKITA, 2016). Makala yamebaini kuwa miongoni mwa mbinu nyingine ya kibalagha ambayo hutumiwa na Samia katika hotuba zake ni mbinu ya masimulizi ya hadithi. Katika utafiti uliozaa makala haya, tumebaini kuwa katika hotuba zake, Samia hutumia mbinu hii ya lugha ili kutoa historia yake na kuongeza nguvu ya ushawishi kuwa hakuna kinachoshindikana na kuonesha ubalagha wa kukumbuka alikotoka. Tazama dondoo hili hapa chini:

- 16) ...Niko nyumbani nikaambiwa unaitwa ikulu, nikasema eehh! Kuna nini mbona mi sipendi kwenda kule mara uhojiwe milangoni, unyanyaswe nini. Nilikuwa **na kigari changu kidogo kibovu kisuzuki** nikawasha nikenda. Nilipofika nikaambiwa unaitwa na Rais, Mungu wangu nini tena? Nilipofika kaniangalia kanambia hebu niambie historia yako. Nikamuelezea, kabla ya kuingia siasa ulikuwa unafanya nini? Nikajieleza akanambia basi

nenda zako, basi nenda zako. Nikatoka jasho linanitoka, nikawasha kigari changu nikaondoka, nikakaa kama siku tatu. Nikaambiwa unaitwa tena ikulu eeh haya. Mara hii nikaenda na kalamu, nikaenda ndio mhemshimiwa, akanambia kuna kitu, kuna kazi nataka nikutume, nikamwambia sawa, nitume. Tayari nimeishatoa *notebook* na kalamu nataka *ku-note down* kazi ninayotaka kutumwa...akanambia nataka unisaidie kwenye nafasi ya Waziri wa Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Nikamwambia heee!! Mbona kubwa hiyo?

Hivyo niseme kwamba ukiona **vinaelea vimefanyaje? ... vimeundwa** (hadhira ikaitikia). Sasa basi ninapokea heshima hii kwa ajili yangu mimi, naipokea kwa ajili ya Watanzania woote wanaoendelea kunipa moyo na ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu kama mkuu wa nchi. Lakini aliyeniunda nikafanya yote yale yupo hapa, kwa hiyo PhD hii pamoja *na-dedicate* kwa wote, ***special dedication* kwa boshi wangu Mheshimiwa Rais Mstaafu Amani Abeid Karume**. Ni chini ya uongozi wake ndio nimeweza kufanya yote yale, kwa hivyo nakushukuru sana Rais Mstaafu kwa malezi na miongozo uliyokuwa unanipa na leo malezi yale na miongozo imezaa heshima hii kubwa ambayo nimepewa...

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Mahafali ya Chuo cha Taifa cha Zanzibar-Tunguu, 28 Desemba 2023

Pia, masimulizi ya hadithi katika hotuba za Samia yanadhihirika katika dondoo lifuatalo:

- 17) ...Waarabu wanasema, **Annassu Shahidu Ilaha**, watu ndio mashahidi wa Mungu. Watu wanavyokuongelea Mungu nae anapokea. Nitakupeni mfano, mnakumbuka kulikuwa na Bunge la Katiba, nadhani katika maisha yangu, katika kazi niliyoifanya ilikuwa ngumu na niliifanya vizuri ilikuwa kazi ile. Lakini wakati tunafunga Bunge mtu mmoja, Paulo Makonda, akasema, wagombea mnaogombea urais ikikupendezeni huyu mama kwa kazi aliyofanya hapa anafaa kuwa Makamu wa Rais, Bunge lote likapokea na wakati ule Mungu alikuwa anawasikia - alimsikia Makonda, alisikia Bunge lilivyopokea, **Annasu Shahidu Ilah**, watu ni mashahidi wa Mungu, kwa hivyo, chungu sana watu wasikuongee vibaya...

Chanzo: Hotuba ya SSH jijini Dodoma, 3 Agosti 2020

Katika dondoo la 16 na 17 tunabaini kuwa Samia ametumia mbinu ya kusimulia hadithi ili kufafanua hatua mbalimbali za maendeleo alizopiga katika shughuli zake za uongozi na siasa. Katika masimulizi tumebaini kwamba alitumia misemo ya lugha ya kigeni kama vile ***Annasu shahidu Ilah, special dedication*** pia methali

kama vile *ukiona vyaalea*... yote ni kwa ajili ya kusimulia hadithi ambazo zimejitokeza katika maisha yake. Ndani ya hadithi hizi kuna mbinu za kibalagha kadhaa ambazo humfanya msikilizaji kuvutiwa na kujifunza kutokana na simulizi hizo. Uteuzi wa mbinu hii hulinda staha za wasikilizaji kwani husema kile kitu ambacho ni sahihi kwa mujibu wa hadithi inayosimuliwa.

4. 8 Kuchanganya Msimbo

Kwa mujibu wa Abdallah (2018), kuchanganya msimbo ni mbinu ya mazungumzo ambapo mzungumzaji huchanganya lugha zaidi ya moja. Aidha, anaendelea kudai kuwa mbinu hii imeenea miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na athari ya elimu. Lugha zote mbili hutumika kuanzia katika ngazi ya sekondari, hali za watu kutaka kuonesha kuwa ni wasomi. Katika makala haya imebainika kuwa mbinu ya uchanganyaji msimbo ilitumiwa kama mbinu muhimu ya kuivuta hadhira na kujenga staha kwa jamii mahususi. Chunguza dondoo lifuatalo:

- 18) ...Maana kuna mtu linakusumbua, kila ukigeuka lipo, ukigeuka lipo linakusumbua achana nae.. **your life is yours, that's the only gift, nani, God gave to you**...maisha yako ni yako mwenyewe ndio zawadi pekee Mungu kakupa..."

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Mkutano na Viongozi wa TAHLISO na ZAHLIFE-Ikulu Dodoma, 11 Februari 2023

Vilevile, mbinu ya kuchanganya msimbo katika hotuba za Samia inadhihirika katika dondoo hili:

- 19) ...Nataka kusema katiba hii ni ya Watanzania si ya vyama vya siasa, kwa hiyo tutakapokuja kuunda kamati kutushauri twendeje itaingiza Watanzania na nyanja zote humu. Kutakuwa na vyama vya siasa humo, tutakuwa na vyama vya kijamii, Watanzania waliopo katika **international communities**, wawakilishi wa vyombo vya ulinzi na usalama **all works of...**

Chanzo: Hotuba ya SSH katika Mkutano na Wadau wa Siasa-Ikulu Dar es Salaam, 31 Januari 2023

Katika dondoo la 18 tunabaini kuwa Samia ametumia mbinu ya kuchanganya msimbo wa Kiswahili na Kiingereza kwa kusema *your life is yours, that's the only gift, nani, God gave to you*... kuonesha umahiri wake wa lugha. Pia, muktadha alimochanganya ndimi au msimbo ulimruhusu kufanya hivyo ili iwe kama njia ya kuwatia shime na uimara wanafunzi aliokuwa akizungumza nao. Muktadha wa wanafunzi hususani wa vyo vikiu, wengi hupenda sana matumizi ya lugha ya Kiingereza, hivyo, alitumia mbinu hiyo ya kibalagha mahususi kufikisha ujumbe alioukusudia ueleweke vyema.

Ama katika dondoo la 19 Samia alichanganya maneno *international communities, all of works* kama mbinu ya kibalagha na kuonesha kuwa mchakato huo wa katiba hautahodhiwa na makundi fulani pekee. Kwa kuwa ni mlumbi na mbuji wa lugha imebainika kwamba mbinu hii huitumia sana.

5.0 Hitimisho

Kwa ujumla, shabaha ya makala haya ilikuwa kuchunguza ujitokezaji wa mbinu za kibalagha na dhima yake katika hotuba za Samia. Matokeo katika makala yamebainisha mbinu anuwai za kibalagha anazoitumia katika hotuba zake. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya viwakilishi vya nafsi za umoja na wingi, tafsida au mafumbo, misemo ya hekima, vitambulisho hadhi, takriri, ufutuhi, masimulizi ya hadithi na kuchanganya msimbo. Aidha, matokeo yamedhihirisha kuwa hutumia lugha hii ya ushawishi katika kuwasilisha masuala anuwai kwa Watanzania. Miongoni mwayo ni kuhimiza umoja na mshikamano, kuonya juu kutumia lugha za staha, kuepuka majungu na fitina, kutoa historia yake, kuonesha mwelekeo wa serikali yake na kuonya juu ya masuala mbalimbali. Makala yamebaini pia kuwa matumizi mazuri ya mbinu za balagha yanaweza kuondosha migogoro, fitina na uvunjifu wa amani katika jamii. Mwito ni kwa viongozi wengine kuiga mfano bora wa Samia katika kutumia lugha inayojali hisia za wasikilizaji wake.

Marejeleo

- Abdallah, M. S. (2018) *Chimbuko la Lugha Tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu na Athari zake kwa Jamii*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.
- Aduradola, R. na Ojukwu, C. (2013) "Language of Political Campaigns and Politics in Nigeria." *Canadian Social Science*, Juz. 9(3):104-116.
- Ayala, S. P. (2001) "FTAs and Erskine May: Conflicting Needs?-Politeness in Question Time". *Journal of Pragmatics*, Juz. 33:143-169.
- BAKITA (2016) *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Press.
- BAKIZA (2010) *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Beom, K. (2010) "Face Threatening /Supporting Strategies in Korean and American TV Presidential Debates: A cultural Comarative Study". *International Association for Intercultural Communication Studies*, Juz. XIX(2):1-21. Inapatikana katika <https://www-s3-live.kent.edu/s3fs-root/s3fs-public/file/01KhisuBeom.pdf>. Ilisomwa tarehe 16 Desemba 2019.
- Bramley, N. R. (2001) "Pronouns of Politics: The Use of Pronouns in the Construction of 'self' and 'other' in Political". Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kitaifa cha Australia, Canberra.
- Brown, G. na Gilman, P. (1960) "The Pronouns of Power and Solidarity". Katika T.A. Sebeok (Mh.) *Style in Language*. Cambridge: The MIT Press. kur. 253-276.

- Chalamila, A. (2011) *Uchanganyaji na Ubadilishaji Msimbo katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu Mwaka 2010*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Grice, H. P. (1975) "Logic and Conversation". Katika P. Cole na J. Morgan (Wah.) *Syntax and Semantics 3*. New York: Academic Press. kur 41-58.
- Habwe, J. H. (2010) *Politeness, Pragmatics and Culture*. Beijing: Foreign Language Teaching and Research Press.
- Hill, B., Ide, S., Ikuta, S., Kawasaki, A. na Ogino, T. (1986). "Universals of Linguistic Politeness: Qualitative Evidence from Japanese and American English". *Journal of Pragmatics*, 10 (3): 347-371.
- Huang, Y. (2008) "Politeness Principle in Cross-Culture Communication". *English Language Teaching*, Juz. 1(1): 96-101.
- Jomo Kenyatta Foundation (2016) *Kamusi Elezi ya Kiswahili*. Nairobi: English Press Ltd.
- Lupogo, I. na Ambrosi, A. (2023) "Mnasaba wa Kipindi cha Uongozi wa Mwalimu Nyerere na Kutangazwa kwa Siku ya Kiswahili Duniani". Katika S. Omari na A. Buberwa (Wah.) *Kiswahili katika Nyanja za Kimataifa*. Dar es Salaam: TUKI. kur. 142-160.
- Lwaitama, A. F. (1988) "Variations in the Use of Personal Pronouns in the Political Oratory of J.K. Nyerere and A.H. Mwinyi". *Belfast Working Papers in Language and Linguistics*, Juz. 1: 1-23.
- Man, P. D. (1984) "Epistemology of Metaphor". Katika Michael J. Shapiro (Mh), *Language and Politics*. New York: New York University Press.
- Mathews, P. H. (1997). *The Concise Oxford Dictionary of Linguistics*. New York: OUP.
- Mulokozi, M. M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi ya Fasihi Vyuho na Vyuho Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.
- Mwansoko, H. J. M. (1994) *Mitindo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Nokkonen, S. (2006) "The Semantic Variation of NEED T in Four Recent British English Corpora". *International Journal of Corpus Linguistics*, Juz. 11(1): 29-71.
- Sovu, A. Y. (2020) *Uchanganuzi wa Mbinu za Kisarufi na Kibalagha katika Vilongo Teule vya Kampeni za Uchaguzi wa Mwaka 2015 Nchini Tanzania*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Sylvester, J. (2016) *Uchanganuzi Kilongo wa Kauli zenye Kutweza au Kukweza Staha katika Mijadala ya Bunge*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- TUKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press.
- Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi*. Vide-Muwa Publishers: Nairobi. www.ikulu.go.tz